KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 12, Issue 5

28th SHA'BAAN 1432

29th July, 2011

YALIYOMO

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUM[Prt.3] 1 - 4

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUMU [Pt. 3]

NIYA KATIKA KUFUNGA

(33) Niya ni sharuti linalohitajika katika saumu za faradhi, na katika saumu nyengine za faradhi kama vile kulipa saumu ulizowacha kuzifunga au saumu zinazofungwa za Kafara, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hakuna saumu kwa mtu ambaye hakutia niya kuanzia usiku uliopita* (Imepokewa na Abu Dawood, no. 2454. Idadi ya wanavyuoni, kwa mfano al-Bukhaari, an-Nasaa'ee, at-Tirmidhee na wengineo walidhania yakwamba imeelekea kuwa kama mawqoof. Angalia katika Talkhees al-Hubayr, 2/188). Niya inaweza kunuiliwa wakati wowote katika usiku, hata kama pia ni muda mchache kabla ya Alfajiri. Maana ya Niya ni kukusudia jambo ndani ya moyo kufanya kitu Fulani, kuitamka Niya hiyo ni bid'ah (uzushi wenye kukemewa), na yoyote ajuae yakwamba kesho ni mojawapo ya masiku ya kufunga basi na atie Niya (Majmoo' Fataawa Shaykh al-Islam, 25/215). Iwapo mtu ataazimia kuvunja saumu yake katika wakati wa mchana lakini kisha asifanye hivyo, basi kulingana na rai iliyokaribu na usawa, saumu yake haikuathirika vibaya na jambo hili; yeye ni kama mtu aliyetaka kuzungumza katika wakati wa swala lakini asifanye hivyo. Baadhi ya wanavyuoni wanadhania yakwamba yeye hafungi muda mchache tu baada ya kuikomesha Niya yake, kwahivyo, ili kusalimika itambidi ailipe saumu hiyo baadae. Hatahivyo, ukanushaji wa Dini hubatilisha Niya, hapana shaka kuhusu suala hili. Mtu mwenye kufunga Ramadhân hana haja ya kuirudia Niya yake katika kila usiku wa Ramadhân, inatosheleza kuwa na Niya mwanzoni mwa mwezi. Iwapo Niya itakatizwa kwa kuvunja saumu kutokana na Safari au maradhi - kwa mfano - itambidi atie Niya upya ya kufunga endapo sababu ya kuvunja saumu itakosekana.

(34) Kutia Niya katika usiku uliopita si katika sharuti za saumu za ujumla za nafl (Sunnah), kutokana na hadeeth iliyopokewa na 'Aa'isha (رضي الله عنها) aliyesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliniingilia nyumbani kwangu siku moja na akasema, 'Muna (chakula) chochote leo?'. Tukasema, 'Laa'. Akasema, 'Kwahivyo mimi nitafunga.'" (Imepokewa na Muslim, 2/809, 'Abd al-Baaqi). Lakini katika hali ya saumu maalum ya nafl kama vile saumu ya 'Arafah na 'Aashooraa', ni bora kuwa upande wa usalama na kutia Niya usiku uliopita.

(36) Iwapo mtu ataanza kufunga saumu ya faradhi, kama vile saumu ya kuilipa siku uliyokosa ya Ramadhân au saumu ya Fidiya, au kufunga kama kitendo cha kulipa kosa (Kafaarah), itamlazimu aikamilishe saumu, na haruhusiwi kuivunja mpaka awe na sababu ifaayo ya kufanya hivyo. Katika hali ya saumu ya naafil, "Mtu mwenye kufunga saumu ya Sunnah ana khiyari emma kuikamilisha saumu yake au kuivunja." (Imepokewa na Ahmad, 6/342) – hata kama hapana sababu ya kuivunja. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema aliamka akiwa amefunga siku moja, kisha akala (kama ilivyopokewa katika Swaheeh Muslim, kuhusu kisa cha al-hais (sampuli fulani ya chakula) alichopewa kama zawadi pindi alipokuwa kwenye nyumba ya 'Aa'isha); No. 1154, 'Abd al-Baaqi). Jee, mtu mwenye kuvunja saumu yake bila ya sababu yoyote atalipwa wema kwa saumu aliyoikamilisha? Baadhi ya wanavyuoni wanasema hatolipwa wema (al-Mawsoo'ah al-Fiqhiyyah, 28/13), kwahivyo ni bora kwa mwenye kufunga saumu ya Sunnah aikamilishe, isipokuwa ikiwa atakuwa na sababu ya mkazo kwake ya kuwacha kufunga.

(36) Iwapo mtu hajui yakwamba Ramadhân imeanza mpaka baada ya alfajiri, atalazimika kuwacha kula na kunywa katika sehemu iliyobaki ya siku, na itambidi ailipe siku hiyo baadae, kulingana na wanavyuoni wengi, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hakuna saumu kwa asiyekuwa na Niya ya kufunga kuanzia usiku uliopita."* (Imepokewa na Abu Dawood, 2454).

(37) Iwapo mfungwa au mateka anajua yakwamba Ramadhân imeanza kwa kujionea mwezi kwa macho yake au kwa kuambiwa na mtu

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

JIPATIE KITABU CHA

"SAUMU YA MWEZI WA RAMADHÂN KAMA ILIVYOTEKELEZWA NA MTUME (صلى الله عليه وسلم)."

TUPIGIE SIMU KATIKA NAMBA HIZI:

+254- 0721473181 AU

+254-0727341779

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

muaminifu, itambidi kufunga. Iwapo yeye atakuwa hajui ni lini utakapoanza mwezi, itamlazimu ajitahidi yeye mwenyewe na atekeleze kulingana na anavyodhani kuwa ni sawa. Iwapo baadae atagundua yakwamba kufunga kwake kunalingana na Ramadhân, hili ni sawa kulingana na wanavyuoni wengi wa fiqh, lakini iwapo atakuwa amefunga kabla ya kuingia Ramadhân, hili halikubaliki na itambidi ailipe siku hiyo. Iwapo sehemu ya saumu yake italingana na Ramadhân na sehemu nyengine haikulingana, kilicholingana nayo au kilichokuja baada yake itakuwa ni sawa, lakini kilichokuja kabla HAIJUZU. Iwapo mas'ala hayatodhihiri kwake, basi saumu yake itakuwa sawa kwa sababu alifanya bidi kadiri ya uwezo wake, na Allaah Haikalifishi nafsi ya mtu zaidi ya uwezo wake. (Al-Mawsoo'ah al-Fiqhiyyah, 28/84).

KUANZA NA KUMALIZA SAUMU

(38) Pindi mkate mzima wa Jua unapopotea, mwenye kufunga na afungue saumu yake, na wala asijali kuhusu wekundu unaobaki kwenye upeo, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Utakapotokeza usiku kutoka upande huu (Mashariki), na ukaondoka mchana kutoka upande huu (Magharibi), na jua likazama, basi atakuwa amefungua mwenye kufunga."* (Imepokewa na al-Bukhaari, al-Fath, No. 1954; mas'ala hayo pia yametajwa katika Majmoo' al-Fataawa, 25/216). Sunnah ni kuharakisha kufungua saumu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa haswali Maghrib mpaka afunguwe saumu yake, hata kama ni kwa tama la maji." (Imepokewa na al-Haakim, 1/432; al-Silsilat as-Swaheehah, 2110). Iwapo mwenye kufunga ameshindwa kupata chochote cha kufungulia saumu yake, na anuilie kufunguwa kwenye moyo wake, na wala asifyonze kidole chake, kama wafanyavyo baadhi ya watu. Na ajitahadhari asifungue saumu yake kabla ya wakati wa sawa, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaona baadhi ya watu wameangikwa kwa visigino vyao na huku damu zikiwatoka kwenye ncha za midomo yao, na alipouliza kuwahusu wao, aliambiwa yakwamba hao ni watu waliokuwa wakifungua saumu zao kabla ya wakati ufaao." (Hadeeth hii yapatikana kwenye Swaheeh Ibn Khuzaymah, no. 1986, na katika Swaheeh at-Targheeb, 1/420). Iwapo mtu atakuwa na yakini, au atadhani huwenda ikawa, au asiwe na hakika kama alifungua saumu yake kabla ya wakati ufaao, itambidi ailipe saumu yake baadae, kwa sababu nguzo ya msingi ni kwamba siku ingalipo na haijesha. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/287). Na ajitahadhari na kutegemea maneno ya watoto wadogo au asili zisizoaminika, na pia ajitahadhari na ikhtilafu za nyakati baina ya Miji tafauti na mitaa anaposikiya miadhini katika Maredio na kadhaalika.

(39) Iingiapo alfajiri - ambayo ni muangaza mweupe unaotokeza kutoka kwenye upeo wa sehemu za Mashariki - itamlazimu mwenye kufunga kukoma kula na kunywa hapohapo, emma atasikiya muadhini au hatosikiya. Iwapo atajua yakwamba muadhini ataadhini alfajiri, itambidi akome kula na kunywa pindi tu atakaposikiya muadhini wake, lakini kama muadhini ataadhini kabla ya Fajr, hatokuwa na haja ya kukoma kula na kunywa atakapousikiya. Iwapo atakuwa haelewi kawaida za mwenye kuadhini au kuna ikhtilafu baina ya wenye kuadhini, na akawa yeye binafsi hawezi kutambua wakati wa alfajiri uingiapo - kama ilivyo hali ya kawaida kwenye Miji ya Mataa na Majumba makubwa – na achukuwe hadhari katika orodha ya mpangilio wa nyakati (Time-table), maadamu yeye atakuwa na hakika yakwamba hesabu za nyakati zilizotegemezwa juu yake hazina makosa. Fikra ya kuwa kwenye upande wa usalama kwa kukoma kula na kunywa wakati fulani kabla ya Fajr, kama vile dakika kumi kabla, ni BID"AH. Kwenye baadhi ya hizi Time-table utaona kichwa kimoja kilichoandikwa "Imsaak" (kukoma kula na kunywa) na nyengine ya Fajr, hili ni jambo lendalo kinyume na Uislamu.

(40) Waislamu wanaoishi kwenye Miji ambayo kuna mabadiliko tafauti ya usiku na mchana katika kila muda wa masaa ishirini na nne wanawajibika kufunga, pasi na kujali urefu wa siku, maadamu tafauti hiyo ya usiku na mchana itaendelea kupatikana. Katika baadhi ya sehemu hakuna tafauti kama hiyo baina ya usiku na mchana, Waislamu katika sehemu hizo na wafunge kulingana na nyakati za Miji iliyokurubiana nao ambazo kunapatikana nyakati tafauti za usiku na mchana.

MAMBO YENYE KUHARIBU SAUMU

(41) Mbali na Heidh (damu ya mwezi) na nifaas (damu ya mazazi), mambo mengine yenye kuharibu saumu

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

TANGAZO LA DARSA ZA RAMADHÂN 2011/1432H

MASJID MAZRUI [KILA SIKU BA'DA SWALAAT ADH-DHUHR]

JUMATATU HADI JUMATANO / [Nawaaqidh ul-Islaam] / Ustadh Athman Bin Na'man

ALKHAMIS / [-] / Ustadh Sharrif

JUMAMOSI NA JUMAPILI / [AL-WAABIL AS-SWAYYIB] / Abu 'Abdur-Razzaq Haruna Rass.

DARSA ZA WANAWAKE MASJID MAZRUI NI KILA SIKU [ISIPOKUWA IJUMAA] KUANZIA SAA NNE ASUBUHI MPAKA SAA SITA.

MASJID KHAYRAAT [KIZIWI] [BA'DA SWALAAT ADH-DHUHR]

JUMANNE NA ALKHAMIS / [Ustaadh Muhammad Abdillah]

JUMATANO / [TAS-HEEL AL-AQEEDAH] / Abu Abdur-Razzaq Haruna Rass.

Unaweza kusikiliza Darsa hizi kwenye Mtandao (Internet)

Pal-Talk ⟹ All-Rooms ⟹ Religion & Spirituality ⟹ Islam ⟹ Callers to Tawheed ⟹ Swahili Duroos.

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

huzingatiwa kufanya hivyo iwapo masharuti matatu peke yake yafuatayo yatapatikana: Ikiwa mtu anajua yakwamba jambo fulani linaharibu saumu na si mjinga wa hilo; Ikiwa anajua alifanyalo na hakusahau yakwamba amefunga,; Ikiwa atafanya jambo kwa khiyari yake mwenyewe na hakulazimishwa.

Miongoni mwa mambo yenye kufunguza saumu ni vitendo vyenye kuhusiana na utoaji wa maji mwilini, kama vile tendo la kujamiiana, kutapika, heidh na kuumika, na vitendo vyenye kuhusisha uakiaji, kama vile kula na kunywa. (Majmoo' al-Fataawa, 25/148).

(42) Miongoni mwa mambo yenye kuharibu saumu ni mambo yaliyo orodheshwa kuwa kama kula au kunywa, kama vile kula dawa na tembe kwa kupitia mdomoni, au sindano zenye madini ya virutubishi, au upaji wa damu. Sindano ambazo zisizotolewa badala ya chakula na kinywaji lakini zenye kutumiwa kuendesha madawa kama vile penicillin na insulin, au dawa ya kuchangamsha mwili, au chanjo, haziharibu saumu, bila ya kujali iwapo ni ndani ya misuli au ndani ya mishipa. (Fataawa Ibn Ibraaheem, 4/189). Lakini ni bora kwa usalama, sindano zote hizi zitumiwe katika wakati wa usiku. Usafishaji damu kwa mashini ya figo (Kidney dialysis), ambapo damu hutolewa, ikasafishwa, na ikarudishwa ikiwa na kemikali au madini ya virutubishi kama vile nyongeza za sukari na chumvi, huzingatiwa kuwa ni vyenye kuharibu saumu. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/190).

Kulingana na rai iliyo karibu na usawa, vidonge vya kutiwa kwenye tupu, dawa za macho, dawa za masikio, kung'olewa jino na kutibu vidonda haziharibu saumu. (Majmoo' Fataawa Shaykh al-Islam, 25/233, 25/245). Vivutia-hewa (Puffers au Inhalers) kwa ugonjwa wa Pumu haziharibu saumu, kwa sababu hizi ni vishindikizi vya hewa iliyobanwa hadi kwenye mapafu - si chakula, na inahitajika wakati wote, katika mwezi wa Ramadhân na nyakati nyengine. Kutolewa damu hakuharibu saumu na inaruhusiwa kwa sababu ni jambo lenye kuhitajika (Fataawa al-Da'wah: Ibn Baaz, no. 979). Madawa yenye kutumika kwa njia ya kusukutuwa hayaharibu saumu maadamu hayamezwi. Iwapo mtu atajazwa katika jino lake na akahisi ladha Fulani katika koo yake, hili haliharibu saumu yake. (Kutoka katika fataawa za Shaykh 'Abd al-'Azeez ibn Baaz, zilizotolewa kwa njia ya kauli).

MAMBO YAFUATAYO HAYAHARIBU SAUMU:

- Kutiwa dawa masikioni kwa sirinji, dawa za pua na vipulizo vya Pua (nasal-spray) - maadamu mtu atajiepusha na kumeza chochote chenye kufika kwenye koo.
- Tembe zenye kuwekwa chini ya ulimi kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa moyo unaosababisha maumivu kifuani (angina) na hali nyengine - maadamu mtu atajiepusha na kumeza chochote chenye kufika kwenye koo.
- Chochote chenye kuingizwa ndani ya tupu ya Mwanamke, kama vile kingamimba (pessaries), dawa ya kupiga Bomba (douches), scopes au vidole kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu.
- Kutia chombo cha kufanyia utafiti au kitanzi (kidude cha kuzuiya mimba IUD au Coil) na mfano kama huo ndani ya mji wa Uzazi.
- Kuingiza ndani ya tundu nyembamba ya tupu (urethra) - kwa wanaume au wanawake - bomba jembamba sana (catheter) kwa ajili ya kutolea uchafu mwilini, opaque dye kwa kuchunguza na kubainisha magonjwa, utabibu au myeyusho wa kusafisha kibofu cha mkojo.
- Kujazisha meno, kung'oa meno, kusafisha meno, kutumia siwaak au msuaki - maadamu mtu atajiepusha na kumeza chochote chenye kufika kwenye koo.
- Kuosha mdomo, kusukutuwa au kutia spray ya mdomo maadamu mtu atajiepusha na kumeza chochote chenye kufika kwenye koo.
- Sindano ya chini ya ngozi, ndani ya misuli au ndani ya mishipa isipokuwa kwa zile zinazotumika kwa ajili ya kuongeza virutubishi.
- Hewa ya Oxygen, hewa za ganzi - madamu mgonjwa hapewi mchanganyiko wa virutubishi. Madawa yanayoingia kwa kupitia kwenye ngozi, kama krimu na bendeji zenye kuhifadhi madawa na kemikali.
- Kuingizwa bomba nyembamba ndani ya mishipa kwa ajili ya uchunguzi au kutibu viini vya damu vilivyomo ndani ya moyo au viungo vyengine.
- Matumizi ya laparoscope (chombo kiingizwacho kupitia kwenye mkato mdogo katika sehemu ya tumbo) kwa ajili ya kuchunguza mvungu wa tumbo au kufanya upasuaji.
- Kuchuna baadhi ya sehemu za mwili au kutoka katika lni au sehemu nyengine - maadamu hili halitoandamana na kutumia michanganyiko.
- Gastroscopy - maadamu hili halitoandamana na kutumia michanganyiko.
- Kuingizwa chombo chochote au tiba kwenye ubongo au Uti wa mgongo.

(43) Mtu yoyote atakaekula au kunywa kwa makusudi katika mwezi wa Ramadhân bila ya sababu ifaayo amefanya madhambi makubwa (kabeerah), na itambidi atubie na ailipe siku hiyo baadae. Iwapo atakuwa amevunja saumu yake na kitu cha Haraam, kama vile kunywa pombe, hili litafanya madhambi yake kuwa maovu zaidi. Kwa hali yoyote iwayo, itambidi atubie kwa unyenyekevu na atekeleze vitendo vingi vya nawaafil, kufunga na vitendo vyengine vya 'Ibaada ili apate kujiepusha na kila aina ya upungufu katika amali zake za faradhi na ili Allaah amtakabalie msamaha wake.

(44) "Iwapo atasahau, na akala na akanywa, basi muache akamilishe saumu yake kwani Allaah amemlisha na akampa anywe." (Imepokewa na al-Bukhaari, Fath, no. 1933). Kulingana na riwaya nyengine, "Hatokuwa na haja ya kulipa baadae au kulipa Kafaarah." Iwapo mtu atamuona mwenzake anakula kwa sababu amesahau yakwamba amefunga, na amkumbushe, kwa sababu ya ujumla wa maana ya aya (Maana ya tafsiri): **"... Saidianeni katika al-Birr (wema) na Taqwaa (uchaji) ..."** [al-Maa'idah 5:2], na hadeeth , "iwapo nitasahau, nikumbusheni." na kwa sababu ya msingi ambao ni, Jambo ovu (munkar) ambao hauna budi kubadilishwa. (Majlis Shahr Ramadhân, Ibn 'Uthaymeen, p.70)

(45) Wale wenye kutaka kufungua saumu zao ili wapate kumsaidia mtu ambaye maisha yake yako hatarini, wanaweza kuvunja saumu zao na walipe katika siku zijazo. Hili linawezekana katika hali ambayo mtu anazama, au moto unapohitajika kuzimwa.

(46) Ikiwa mtu anawajibika kufunga,

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

lakini akajamiiyana na mkwewe kwa makusudi katika mchana wa Ramadhân, kwa mapendeleo yake mwenyewe, ambapo tupu mbili "zilizotahiriwa" (tupu) ziligusana na sehemu ya ncha ya tupu ya mwanamume ikazama ndani ya njia ya emma mbele au nyuma, saumu yake imevunjika, emma awe ametokwa na manii au laa, na atawajibika kutubia. Itamlazimu aendelee kufunga katika sehemu iliyobaki ya siku hiyo, lakini itambidi ailipe saumu hiyo baadae, na atoe kafaarah, kwa sababu ya hadeeth iliyopokewa na Abu Hurairah (رضي الله عنه): Yakwamba mtu mmoja alikuja kwake akasema: "Yaa Rasoolullaah mimi nimeangamia." Akamuuliza: "Ni lipi lililokuangamiza?" Akasema: "Mimi nimemuingilia mke wangu katika mchana wa Ramadhân." Akamuuliza: "Waweza kuacha huru mtumwa?" Akamjibu: "Laa." Akamuuliza: "Jee, waweza kufunga miezi miwili mfululizo?" Akajibu: "Laa." Akamuuliza: "Jee, waweza kulisha maskini sitini?" Akamjibu: "Laa." Akasema: "Basi keti hapa." Akaketi pale. Mara Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaletewa tagaa la tende na akamwambia yule mtu: "Nenda ukatoe hii kama swadaka." Yule mtu akasema kumwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Baina ya miji miwili hii hakuna fakiri kuliko sisi." Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaanza kucheka mpaka meno (magego) yake yakawa ni yenye kuonekana, akasema: "Haya chukuwa uwende ukawalishe watu wako." (Reported by al-Bukhaari, al-Fath, 4, no. 1936). Hukmu kama hiyo pia inatumika katika hali ya zinaa, uliwati na kumuingilia mnyama. [Nukta ya Mfasiri: Kuingiliana kwa njia ya nyuma, uzinifu, uliwati, na kufanya tendo la kuingiliana na mnyama ni miongoni mwa madhambi makubwa katika Uislamu na huzidi ukubwa wake iwapo yatafanywa katika mchana wa Ramadhan.] Iwapo mtu atafanya tendo hilo la kuingiliana kimapenzi katika mchana kwa zaidi ya siku moja katika mwezi wa Ramadhân, itamlazimu alipe kafaarah kwa kiloa siku moja, pamoja na kuzilipa saumu kwa kila siku. Kutojua yakwamba Kafaarah ni waajib haijakuwa ni sababu. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/321).

(47) Iwapo mtu ataka kumuingilia mkewe lakini kwanza akavunja saumu yake kwa kula mwanzo, madhambi yake ni makubwa zaidi, kwa sababu atakuwa amekhalifu Utakatifu wa mwezi kwa makosa mawili, kwa kula na kwa kuingiliana na mkewe. Ni kwa yakini kabisa katika hali hii yakwamba Kafaarah ni waajib, na lau atajaribu kuikwepa hukmu hiyo, hilo litazidisha kuyafanya mambo kuharibika zaidi. Ni lazima atubie kihakika. (See Majmoo' al-Fataawa, 25/262).

(48) Kumbusu, kumkumbatia, kumpiga pambaja, kumgusa na kumtupia macho mara kwa mara mkeo au hawara wako, ikiwa mtu aweza kujizuiya, inaruhusiwa, kwa sababu imepokewa katika swaheehayn kutoka kwa 'Aa'isha (رضي الله عنها) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiwabusu na kuwakumbatia wake zake haliyakuwa alikuwa amefunga, lakini yeye alikuwa ndiye mbora katika kujizuiya na kujimiliki na matamaniwa yake. Kuhusiana na hadeeth Qudsi: "Hujiepusha na mkewe kwa ajili Yangu." Hii inahusu kuingiliana kimapenzi. Lakini iwapo mtu huzidiwa na matamaniwa kwa haraka na akashindwa kujimiliki nafsi yake, basi haruhusiwi kumbusu wala kumkumbatia, kwa sababu hilo litamsababisha aharibu saumu yake, kwa vile hawezi kuwa na hakika yakwamba atakuwa na uwezo wa kujiepusha na kutokwa na manii au kumuingilia. Allaah Amesema katika Hadeeth Qudsi: "na akaachana na matamaniwa yake kwa ajili Yangu." Mipaka ya Ki-Islamu ni kwamba kitu chochote chenye kuelekeza kwenye haraam, nacho pia ni haraam.

(49) Iwapo mtu atakuwa kwenye kitendo cha kujamiiyana na alfajiri imeingia, anawajibika kujiondoa hapo, na saumu yake itakuwa sawa, hata kama atatokwa na manii baada ya kuondoka, lakini ikiwa ataendelea na kitendo hicho mpaka baada ya alfajiri, atakuwa ameharibu saumu yake, na itamlazimu kuilipa siku hiyo baadae, na alipe kafaarah.

(50) Iwapo kumepambazuka asubuhi na alikuwa katika hali ya janaba, hili halitoathiri saumu yake. Yeye Mume/ Mke anaruhusiwa kuchelewesha kutekeleza ghusl, emma ilitokana na Janaaba au imetokana na heidh au nifaas, mpaka baada ya jua kuchomoza, lakini ni bora kuharakisha kutekeleza ghusl ili mtu aweze kuswali.

(51) Iwapo mwenye kufunga amelala na katika usingizi wake akaota ndoto na kutoka na manii, hili haliharibu saumu yake kulingana na maafikiano ya wanavyuoni (Ijmaa'), kwahivyo na amalize saumu yake. Kuchelewesha kuoga ghusl hakuharibu saumu ya mtu, lakini na aharakishe kutekeleza ghusl ili apate kuswali na ili Malaika wapate kumkurubia.

(52) Iwapo mtu atatoka na manii katika mchana wa Ramadhân kwa sababu ya jambo ambalo angeliweza kujiepusha nalo, kama vile kumgusa au kumtizama Mwanamke mara kwa mara, itamlazimu atubie kwa Allaah na aendelee kufunga katika sehemu iliyobaki ya siku, lakini vilevile itambidi kuilipa siku hiyo baadae. Iwapo mtu ataanza "ku-Masturbate" lakini kisha akawacha kufanya hivyo, na asitokwe na manii, basi itamlazimu atubie, lakini hatowajibika kuilipa siku hiyo baadae, kwa sababu hakutokwa na manii. Mwenye kufunga ni lazima ajiepushe na kila kitu kiwezacho kumshawishi na matamaniwa na nafsi yake, na ni lazima aondoe fikra mbaya yoyote inayomjia. Hatahivyo, kulingana na rai iliyo karibu na usawa, iwapo atatokwa na madhee, hilo halitomuharibia saumu yake. Kutokwa na wade, maji-maji mazito yatokayo baada ya kumalizika mkojo, bila ya starehe zozote za ki-mwili, haiharibu saumu, na mtu hawajibiki kutekeleza ghusl, lakini ni lazima akafanye istinjaa (akajioshe sehemu zake za siri) na kutawadha. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/279)

NENO LA BUSARA

"

KILA 'IBAADA AMBAYO MASWAHABA WA MTUME (صلى الله عليه وسلم) HAWAKUIFANYA, NA NYINYI MUSIIFANYE.

"

Hudhaifa ibn al-Yamani